

MUHTASARI


- Kipindi cha Septemba, 11-20, 2017, maeneo mengi ya nchi yaliendelea kuwa makavu, isipokuwa maeneo machache ya mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara, Mtwara, Kigoma, Rukwa, Morogoro, visiwa vya Unguja na Pemba, Arusha, Manyara, Tanga, Pwani, Kilimanjaro na Dar es Salaam ambayo yalipata mvua
- Wakulima wanaopata misimu miwili ya mvua waliendelea kuandaa mashamba na kupanda hususan mkoa wa Kagera
- Vipindi vya upepo mkali vinarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kusini
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasababisha upungufu wa maji kwa mifugo, hivyo wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji na malisho.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Katika kipindi tajwa, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu na hivyo kudhoofisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Migandamizo iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) nayo pia iliendelea kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kushuka kuelekea kusini mwa dunia. Joto la juu kidogo ya wastani liliendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) joto la bahari lilikuwa chini ya wastani hadi wastani. Hali hii ilipelekea hali ya ukavu kwa maeneo ya magharibi mwa nchi na yale yaliyopo katika ukanda wa ziwa Viktoria.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa, mvua za msimu wa vuli kuzenye kufikia milimita (mm) 20 na mm 80 zilinyesha katika maeneo mengi ya mikoa wa Kagera, Mwanza na Mara na maeneo machache ya mikoa ya Geita, Simiyu, Manyara, Tanga, Morogoro, na kisiwa cha Pemba kama inavyoonekana katika Kielelezo. Mvua hizi zilinyesha katika maeneo mengi ya ukanda wa ziwa Viktoria kuashiria kuanza kwa msimu wa vuli hususan kwa maeneo ya mkoa wa Kagera. Maeneo mengine ya nchi yaliyosalia yaliendelea kuwa makavu au kupata mvua nyepesi chini ya mm 20.



Kielelezo. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Septemba 11-21, 2017

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli waliendelea na uandaaji wa mashamba isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambapo wameanza kupanda mazao. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kilimo cha msimu. Upatikanaji wa maji na

malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Arusha, Manyara na Dodoma ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua kuliko maeneo mengine nchini.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vililendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu unayoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2017

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu na hivyo kudhoofisha mkondo wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati, ile migandamizo iliyopo sehemu za kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kuendelea kushuka kuelekea sehemu ya kusini mwa Dunia. Joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha upepo wenye unyevu kiasi kuvuma kutoka kusini na kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Kwa upande mwingine, kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki joto la bahari litaendelea kuwa la chini kidogo ya wastani. Hii inatarajiwa kupunguza nguvu ya upepo wenye unyevu kutoka katika msitu wa Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi na kusababisha maeneo hayo kuwa makavu.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa, maeneo mengi yanatarajiwa kuwa makavu yakiambatana na hali ya ubaridi. Maeneo ya **ukanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu)** yanatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache zitakazoambatana na ngurumo. Maeneo ya **nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara)** na **nyanda za juu kusini**

magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache hususan kwenye miinuko. Maeneo ya **Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)** yanatarajiwa kuwa makavu isipokuwa katika maeneo machache ya mkoa wa Tanga na visiwa vya Unguja na Pemba. Maeneo ya **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), Kanda ya kusini (Mikoa ya Njombe na Ruvuma) na kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida)** yanatarajiwa kuwa makavu. Maeneo ya **Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi)** yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache na upepo mkali.

MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2017

Mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha hazitarajiwi kutosheleza uoteshaji wa mazao bali zinaweza kuathiri mavuno yasiyohifadhiwa vizuri isipokuwa kwa mkoa wa Kagera ambapo msimu ya vuli umeanza. Hali ya ukavu inayotarajiwa itaathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa maeneo mengi nchini, hivyo wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito vitaendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255-(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz